

Hifadhi Misitu ya Mteremko wa Udzungwa

Kuhifadhi Misitu ya Mteremko wa Udzungwa ni muhimu kwa ajili ya maisha ya watu wanaoishi katika na kuzunguka Bonde la Kilombero. Misitu ya Mteremko wa Udzungwa inasaidia kulinda mito midogo inayotiririsha maji kwenye Bonde la Kilombero. Misitu hii pia inalinda udongo na kuzuia miporomoko ya ardhi. Misitu hii pia ina mimea na wanyama wengi wa kipekee.



Mteremko wa Udzungwa na si popote duniani. Aina hii ya viumbe ni hadimu sana na vinaweza kupotea kabisa kama misitu hii imeharibiwa.

Misitu hii inatishiwa na uvunaji wa magogo kinyume na sheria na kufyekwa kwa ajili ya ardhi ya kilimo. Kuna aina mbili za wanyama kama kima wanaopatikana Udzungwa tu wako hatarini kutoweka kwa kuwindwa.

Minde (Abbott's duiker)

Minde ni funo wa msituni ambaye yuko kwenye tishio kubwa kutokana na uwindaji. Anapatikana kwenye misitu michache ikiwemo ya milima ya Udzungwa. Kwenye baadhi ya misitu ya Tanzania ambako walikuwa wanapatikana kwa wingi, kama Tanga, wametoweka kabisa kutokana na uwindaji na uharibifu wa msitu

Mbega mweupe kusi (Black and white colobus)

Aina hii ya mbega anapatikana katika Milima ya Udzungwa na si pengine popote duniani. Anakula zaidi majani na hapendelei kabisa usumbufu msituni. Wanasayansi wamegungua kuwa idadi ya aina hii ya mbega imeshuka kutokana na uwindaji na usumbufu katika makazi yao. Kama uwindaji utaendelea kwa kiasi kilichopo sasa, hakutokuwa na mbega wekundu wa Udzungwa katika Misitu ya Mteremko wa Udzungwa miaka michache ijayo.

Mbega mweupe kusi (Black and white colobus)

Aina hii ya mbega anapatikana katika Milima ya Udzungwa na si pengine popote duniani. Anakula zaidi majani na hapendelei kabisa usumbufu msituni. Wanasayansi wamegungua kuwa idadi ya aina hii ya mbega imeshuka kutokana na uwindaji na usumbufu katika makazi yao. Kama uwindaji utaendelea kwa kiasi kilichopo sasa, hakutokuwa na mbega wekundu wa Udzungwa katika Misitu ya Mteremko wa Udzungwa miaka michache ijayo.

Mbega mweupe kusi (Black and white colobus)

Aina hii ya mbega anapatikana katika Milima ya Udzungwa na si pengine popote duniani. Anakula zaidi majani na hapendelei kabisa usumbufu msituni. Wanasayansi wamegungua kuwa idadi ya aina hii ya mbega imeshuka kutokana na uwindaji na usumbufu katika makazi yao. Kama uwindaji utaendelea kwa kiasi kilichopo sasa, hakutokuwa na mbega wekundu wa Udzungwa katika Misitu ya Mteremko wa Udzungwa miaka michache ijayo.

CRITICAL ECOSYSTEM PARTNERSHIP FUND



Mbega mweupe kusi (Black and white colobus)

Mbega hawa walikuwa wengi sana katika Misitu ya Mteremko wa Udzungwa. Kutokana na uwindaji karibu wote wametoweka na unaweza usione Mbega Mweupe Kusi katika Misitu wa Mteremko wa Udzungwa.



Nyoka ya misitu mwenye pua nyekundu (Red-snouted wolf snake)

Nyoka huyu anapatikana tu katika Milima ya Udzungwa.



Moma mwenye pembe (Horned Bush viper)

Aina hii ya nyoka anapatikana tu katika Milima ya Tao la Mashariki. Ana sumu kali na anakula ndege na wanyama wadogo wenye uti wa mgongo.



Chura wa mitini wa Barbour (Barbour's tree frog)

Aina hii ya chura anapatikana tu katika Milima ya Tao la Mashariki. Anaishi kwenye miti.



Chura wa Msituni wa Wendy (Wendy's forest toad)

Aina hii ya chura wanapatikana tu katika bonde moja tu kwenye Hifadhi ya Misitu ya Mteremko wa Udzungwa na si pengine popote duniani. Si kawaida kabisa kuona chura ambao wanaishi katika eneo dogo kama hili la bonde moja tu. Aina hii ya chura wanaathirika na mabadiliko yoyote yanayotokea katika makazi yao.

Picha na Michele Menegon, MTSN.

Misitu. Tuilinde. Itulinde.

Bango hili linaonyesha baadhi ya wanyama waliochukuliwa katika Hifadhi za Misitu ya Mteremko wa Udzungwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania na Makumbusho ya Trento ya Sayansi Asilia, Italia

Bango hili limetayarishwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania kwa ufadhili kutoka Hazina ya Mazingira yaliyo katika Hali ya Kuangamizwa (CEPF)